BENKI KUU YA TANZANIA



Tathmini Ya Mwenendo Wa Uchumi

Septemba 2026

Yaliyomo

1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia.....1

2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa.....3

2.1 Mfumuko wa Bei.....3

2.2 Sera ya Fedha 6

2.3 Viwango vya Riba 8

2.4 Masoko ya Fedha 8

2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali 9

2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa 10

2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje 12

3.0 Mwenendo wa Uchumi Zanzibar 14

3.1 Mfumuko wa Bei 14

3.2 Bajeti ya Serikali 15


3.3 Mwenendo wa Sekta ya Nje 16

VIAMBATISHO 18

1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia


Uchumi wa dunia umeendelea kuwa himilivu ukitarajiwa kukua kwa asilimia 3.0 mwaka 2026[1]. Mahitaji thabiti ya ndani na uwekezaji mkubwa katika akili unde vinaendelea kuimarisha shughuli za kiuchumi katika mataifa yenye uchumi mkubwa duniani. Hata hivyo, mvurugiko katika usafirishaji kupitia Mlango-Bahari wa Hormuz umeongeza hali ya kutotabirika, iliyosababisha kupanda kwa bei za nishati na mbolea, na hivyo kuongeza shinikizo la mfumuko wa bei duniani. Nchi zinazoagiza nishati zimeendelea kukabiliwa na hatari kubwa kutokana na kuzorota kwa uwiano wa biashara , kuongezeka kwa nakisi ya urari wa malipo ya kawaida, na kushuka kwa thamani ya sarafu. Hata hivyo, hali ya kutotabirika kwa sera za uchumi na biashara duniani imepungua ikilinganishwa na viwango vya juu vya mwezi September 2025 (Kielelezo 1.1a na Kielelezo 1.1b).

Kielelezo 1.1a: Fahirisi ya Kutotabirika kwa Sera za Uchumi za Dunia



Chanzo: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Sera za Uchumi Duniani, Septemba 2026 (https://www.policyuncertainity.com/trade)

Kielelezo 1.1b: Fahirisi ya Kutotabirika kwa Biashara Duniani



Chanzo: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Sera za Uchumi Duniani, Septemba 2026 https://worlduncertainityindex.com/

Bei za bidhaa ziliendelea kuonesha mwenendo mchanganyiko mwezi Agosti 2026. Bei ya nishati iliongezeka kufuatia kuibuka tena kwa mgogoro Mashariki ya Kati, hali iliyoongeza gharama za usafirishaji. Bei ya mafuta ghafi iliongezeka kwa asilimia 5.8, na kufikia dola za Marekani 84.4 kwa pipa, kiwango ambacho ni takribani asilimia 36 juu ya wastani uliorekodiwa kabla ya kuanza kwa mgogoro robo ya nne ya mwaka 2025. Bei ya gesi asilia barani ulaya iliongezeka kwa asilimia 16.9 kutokana na kuendelea kwa mvurugiko wa usafirishaji wa gesi asilia iliyochakatwa kupitia Mlango-Bahari wa Hormuz. Bei ya dhahabu iliimarika, ikiongezeka hadi dola za Marekani 4,441 kwa wakia, kutoka dola za Marekani 4,073 kwa wakia mwezi Julai 2026. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuimarika kwa mahitaji ya dhahabu kama hifadhi salama ya thamani kutokana na hali ya kutokuwa na uhakika katika uchumi wa dunia, pamoja na kupungua kwa matarajio ya kuendelea kudhibitiwa kwa sera ya fedha ya benki kuu ya Marekani.


Bei za bidhaa za kilimo zilionesha mwenendo tofauti mwezi Agosti 2026 . Bei za ngano na Sukari ziliongezeka kwa asilimia 6.5 na asilimia 11.8, mtawalia, zikisababishwa na mvurugiko wa usafirishaji kupitia ukanda wa Bahari Nyeusi pamoja na hali mbaya ya hewa. Bei ya kahawa aina ya Arabika iliongezeka kwa asilimia 0.8, kufutia kuchelewa kwa mavuno nchini Brazil na

[1] Shirika la Fedha la Kimataifa, Taarifa ya matarajio ya ukuaji wa Uchumi wa Dunia, Julai 2026.

athari zinazohusishwa na hali mbaya ya hewa, hasa El Nino, wakati bei ya kahawa aina ya Robusta ilipungua kwa asilimia 2.2 ikichangiwa na uzalishaji mkubwa wa kahawa duniani. Bei ya mafuta ya mawese iliongezeka kwa asilimia 1.5, ikichangiwa na mahitaji makubwa na wasiwasi kuhusu kupungua kwa ugavi katika baadhi ya maeneo makubwa ya uzalishaji duniani.

Bei za mbolea zilionesha pia mwenendo mchanganyiko. Bei ya Urea ilipungua kwa asilimia 2.5 kutokana na kupungua kwa mahitaji ya msimu na ongezeko la mauzo ya nje nchini China, huku bei ya DAP iliongezeka kwa asilimia 1.6 kutokana na kuendelea kuwepo kwa changamoto za ugavi katika soko la dunia (Kielelezo 1.2, Jedwali 1.1 na Kiambatisho A8).

Kielelezo 1.2: Bei za Bidhaa Katika Soko la Dunia



Chanzo: Bloomberg

Jedwali 1.1: Bei ya Bidhaa Katika Soko la Dunia

Wastani kwa kila mwezi

Bidhaa	Kizio	Jun-26	Jul-26	Ago-26	Mabadiliko (%)
Mafuta ghafi, wastani	Dola za Marekani/pipa	81.7	79.8	84.4	5.8
Dhahabu	Dola za Marekani/wakia	4,228	4,073	4,411	8.3
Gesi asilia, Ulaya	Dola za Marekani/MMBtu	15.17	18.06	21.11	16.9
Ngano, Marekani HRW	Dola za Marekani/tani	286	310	330	6.5
Sukari, Dunia	Dola za Marekani/kg	0.32	0.34	0.38	11.8
Kahawa , Arabika	Dola za Marekani/kg	6.79	7.91	7.97	0.8
Kahawa, Robusta	Dola za Marekani/kg	3.73	4.07	3.98	-2.2
Mafutaya Mawese	Dola za Marekani/tani	1,104	1,101	1,117	1.5
DAP	Dola za Marekani/tani	783.8	781.3	793.5	1.6
Urea	Dola za Marekani/tani	453.1	400	390	-2.5

Chanzo: Takwimu za Bei za Bidhaa za Benki ya Dunia Septemba 2026.

Tanbihi: DAP inamaanisha fosfati ya diamoniamu mmbtu ni milioni ya vipimo vya joto vya Uingereza; na HRW ni ngano nyekundu ngumu ya msimu wa baridi.

Shinikizo la mfumuko wa bei duniani liliendelea kuwa juu, likiakisi athari za kupanda kwa bei za mafuta zilizopelekea kupanda kwa bei za nishati, usafiri, na bidhaa za kawaida katika nchi mbalimbali. Nchini Marekani, mfumuko wa bei wa jumla ulikuwa asilimia 3.4 mwezi Agosti 2026, ambapo ongezeko la bei za mafuta ya petroli lilisababisha kupungua kwa kasi ya mfumuko wa bei za msingi. Katika eneo la ukanda wa Ulaya, mfumuko wa bei wa jumla uliongezeka hadi asilimia 3.2 kutoka asilimia 2.9 mwezi Julai 2026, ukichangiwa kwa kiasi kikubwa na mfumuko wa bei ya nishati wa asimilia 14.3. Pamoja na mwenendo huu, benki kuu za mataifa makubwa duniani zinategemewa kuendelea kuchukua msimamo wa tahadhari katika kutekeleza sera ya fedha, kutokana na wasiwasi wa kutokea athari za awamu ya pili za ongezeko la gharama za nishati (Kielelezo 1.3).

Kielelezo 1.3: Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi

Asilimia



Chanzo: Bloomberg


Mfumuko wa bei katika nchi zinazoibukia kiuchumi uliongezeka kidogo mwezi Agosti 2026. Nchini China, mfumuko wa bei uliongezeka hadi asilimia 0.8 kutoka asilimia 0.5 mwezi Julai, ukichangiwa na ongezeko la gharama za usafirishaji kufuatia kupanda kwa bei ya mafuta, pamoja na kuongezeka kwa uhitaji wa huduma za usafiri. Nchini India, mfumuko wa bei uliongezeka hadi asilimia 4.8 kutoka asilimia 4.5, ukiakisi, kwa kiasi kikubwa, kupanda kwa bei za chakula.

Mfumuko wa bei katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulikuwa na mwenendo mchanganyiko, ambapo nchi nyingi zilirekodi ongezeko dogo. Kwa

ujumla mfumuko wa bei uliendelea kudhibitiwa na kubaki ndani ya vigezo vya utangamano vya kikanda vilivyokubaliwa, isipokuwa nchi chache (Kielelezo 1.4 na Kielelezo 1.5).

Kielelezo 1.4: Mfumuko wa Bei Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki


Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)

Kielelezo 1.5: Mfumuko wa Bei Miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika

Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)

Matarajio ya hatari ya kudorora kwa uchumi wa dunia yameendelea kuwa juu. Kuendelea kwa mgogoro Mashariki ya Kati kunaweza kuvuruga masoko ya nishati na njia za biashara duniani, kudhoofisha matarajio ya ukuaji wa uchumi, na kuongeza shinikizo la mfumuko wa bei. Hatari zinazohusiana na mabadiliko ya tabia ya nchi zinaendelea kuwa juu. Hali ya El Niño inayotarajiwa kuongezeka zaidi mwishoni mwa mwaka 2026 na mwanzoni mwa mwaka 2027, inaweza kuathiri uzalishaji wa mazao ya kilimo na usambazaji chakula. Hali hiyo inaweza kuongeza hatari ya kupanda kwa bei za vyakula na kuchochea mfumuko wa bei.

2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa

2.1 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei uliendelea kuwa chini na ndani ya lengo la taifa la asimilia 3 hadi 5 na vigezo vya mtangamano wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika. Hata hivyo, mfumuko wa bei wa jumla wa mwaka uliongezeka hadi asilimia 4.3 mwezi Agosti 2026 kutoka asilimia 4.2 mwezi Julai 2026 na juu ya asilimia 3.4 ya mwezi Agosti 2025 (Jedwali 2.1.1 na Kielelezo 2.1.1). Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na athari zilizochelewa kujitokeza za ongezeko la awali la bei za mafuta katika nauli za usafiri wa mabasi, taxi na pikipiki (Kielelezo 2.1).

Hali nzuri ya upatikanaji wa chakula inatarajiwa kudhibiti shinikizo la mfumuko wa bei katika kipindi cha muda mfupi. Hata hivyo, mwelekeo wa mfumuko wa bei bado unakabiliwa na athari za mishtuko ya ugavi, hususan kutokana na ongezeko jipya la bei za mafuta katika soko la dunia linalochangiwa na kuendelea kwa mgogoro Mashariki ya Kati na mvurugiko wa ugavi unaohusiana na hali ya El Niño.

Jedwali 2.1.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei


Asilimia (Kizio: 2020 = 100)

		Badiliko la Mfumuko wa bei (Asilimia)					
		Badiliko: Mwezi hadi Mwezi			Badiliko kwa Mwaka		
Makundi Makuu ya Fahirisi	Mizania	Ago-25	Jul-25	Ago-26	Ago-25	Jul-25	Ago-26
Vyakula na vinywaji baridi	28.2	-0.8	-0.8	-0.3	7.7	4.1	3.7
Vinywaji vikali na tumbaku	1.9	0.1	0.2	0.0	2.9	1.9	1.5
Nguo, mavazi na viatu	10.8	0.0	0.2	0.2	1.7	1.6	1.8
Makazi, maji, umeme, gesi na nishati zinginezo	15.1	-0.4	0.0	0.3	2.1	1.6	2.5
Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa makazi	7.9	0.6	0.4	0.4	2.4	2.2	2.6
Afya	2.5	0.1	0.1	0.0	1.3	1.4	1.5
Usafiri	14.1	0.0	0.1	0.1	1.4	13.8	13.8
Habari na mawasiliano	5.4	0.0	-0.3	0.9	0.4	0.6	1.5
Burudani, michezo na utamaduni	1.6	-0.1	0.0	0.2	1.4	0.7	0.7
Elimu	2.0	0.0	0.1	0.2	3.0	2.8	3.2
Migahawa na huduma za malazi	6.6	0.0	0.8	0.2	0.9	2.7	3.0
Bima na huduma za kifedha	2.1	0.0	0.0	0.0	0.6	0.2	0.2
Huduma binafsi, hifadhi ya jamii na bidha na huduma mchanganyiko	2.1	0.0	-0.1	0.0	2.3	3.4	3.3
Fahirisi bidhaa zote	100.0	-0.3	-0.1	0.1	3.4	4.2	4.3
Makundi mengine teule							
Faharisi ya bidhaa za msingi	73.9	0.1	0.2	0.3	2.0	3.9	4.1
Fahirisi isiyojumuisha fahirishi za bidhaa za msingi	26.1	-1.1	-1.1	-0.4	7.3	4.9	4.8
Fahirisi za mafuta, nishati na bili za maji	5.7	-1.3	-0.8	0.1	2.6	6.9	8.5
Fahirisi za huduma	37.2	0.0	0.4	0.2	0.8	5.7	5.9
Fahirisi za bidhaa	62.8	-0.4	-0.4	0.0	4.9	3.3	3.5
Fahirisi za bidhaa na huduma za elimu	4.1	0.0	0.0	0.2	2.8	1.7	1.8
Fahirisi za bidhaa zote isipokuwa chakula na vinywaji visivyo na kilevi	71.8	0.0	0.2	0.2	1.6	4.2	4.6

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 2.1.1: Mfumuko wa Bei na Malengo yake

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Mfumuko wa bei wa bidhaa za msingi usiojumuisha bei za vyakula visivyochakatwa, nishati na bili za maji uliongezeka hadi asilimia 4.1, kutoka asilimia 3.9 mwezi Julai 2026 na asilimia 2 mwezi Agosti 2025 (Jedwali 2.2.1 na Kielelezo 2.1.2). Mfumuko wa bei wa bidhaa za msingi umekuwa ukiongezeka taratibu tangu mwezi Machi 2026, ikionesha kuongezeka taratibu kwa shinikizo la mfumuko wa bei. Kuongezeka huko kulikuwa sambamba na ongezeko la mfumuko wa bei za huduma, ambao ulifikia asilimia 5.9 kutoka asilimia 0.8 mwezi Agosti 2025. Hata hivyo, mfumuko wa bei wa usafiri ulibaki katika kiwango cha asilimia 13.8, huku shinikizo la mfumuko wa bei likijitokeza pia katika makundi mengine hususan habari na mawasiliano, elimu, pamoja na migahawa na huduma za malazi (Kielelezo 2.1.3).


Kielelezo 2.1.2: Viwango vya Mfumuko wa Bei kwa Miezi Kumi na Mbili

Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 2.1.3: Shinikizo la Msingi la Mfumuko wa Bei




Chanzo : Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Tanbihi : Faharasa za huduma na bidhaa zinajumuisha vipengele vyote vilivyomo katika Kapu la Kielelezo cha Bei za Watumiaji (CPI)

Mfumuko wa bei ya chakula ulipungua hadi asilimia 3.7 mwezi Agosti 2026, kutoka asilimia 4.1 ya mwezi uliotangulia na chini ya asilimia 7.7 iliyorekodiwa mwezi kama huo mwaka 2025 (Jedwali 2.1.1 na Kielelezo 2.1.2). Kupungua huku kuliashiria kuongezeka kwa upatikanaji wa chakula, hususan vyakula vikuu ikiwemo mahindi, mchele, na maharage, ambavyo bei zake zilikuwa chini ya viwango vya mwaka uliotangulia (Kielelezo 2.1.4a, na Kielelezo 2.1.4b).


Kielelezo 2.1.4: Mabadiliko ya Mwaka ya Bei za Jumla za Mazao

a. Mazao ya Vyakula Vikuu



Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

b. Mazao ya Vyakula Mbadala



Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Akiba ya chakula iliyohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ilifikia tani 484,332 mwishoni mwa mwezi Agosti 2026, ikilinganishwa na tani 537,571 mwishoni mwa mwezi Agosti 2025. Katika kipindi cha mwezi Agosti 2026, Wakala ilinunua tani 89.5 na kuuza tani 2,813.7 za mahindi na mpunga kwa wafanyabiashara (Jedwali 2.1.2).

Hatari za kupanda kwa bei za vyakula zinaendelea kuwepo. Mvua za vuli zinazotarajiwa kuwa juu ya wastani kutokana na athari za El Niño zinaweza kuvuruga usafirishaji na usambazaji wa bidhaa za chakula katika maeneo mbalimbali nchini, wakati hali ya ukame kusini mwa Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika inaweza kuongeza mahitaji ya chakula.

Jedwali 2.1.2: Akiba ya Chakula Iliyohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula


Tani

Kipindi	2022	2023	2024	2025	2026
Jan	207,899	124,736	270,984	646,480	567,469
Feb	203,297	106,881	326,172	619,659	560,008
Mac	200,626	80,123	336,099	587,062	533,634
Apr	190,366	63,808	340,102	557,228	510,927
Mei	149,402	51,367	340,002	509,990	500,692
Jun	141,576	46,665	340,479	477,923	489,998
Jul	140,695	94,088	368,855	485,930	487,056
Ago	144,410	210,020	489,187	537,571	484,332
Sep	149,044	244,169	651,403	570,519	
Okt	151,794	244,289	708,399	593,485	
Nov	147,401	244,223	702,502	590,425	
Des	137,655	248,282	677,115	577,376	

Chanzo: Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula

Mfumuko wa bei ya nishati, mafuta na huduma za msingi uliongezeka hadi asilimia 8.5 mwezi Agosti 2026, kiwango cha juu zaidi tangu mwezi October 2024, likichangiwa zaidi na kupanda kwa bei za mkaa na kuni (Jedwali 2.1.1 na Kielelezo 2.1.2). Hali hii ilitokea licha ya kushuka kwa bei za mafuta nchini, ambapo bei za petroli na dizeli jijini Dar es Salaam zilibaki chini ya viwango vya mwezi Juni 2026 (Kielelezo 2.1.5). Hata hivyo, kupanda kwa bei za bidhaa za mafuta ya petroli kunaweka hatari za kupanda kwa mfumuko wa bei wa nishati nchini katika kipindi kijacho.

Kielelezo 2.1.5: Bei za Bidhaa za Mafuta




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Bidhaa nyeupe za petroli huashiria wastani wa bei za Dunia

Mfumuko wa bei wa msingi uliendelea kuwa na mchango mkubwa kwenye mfumuko wa bei wa jumla, ukichangia asilimia 3.1 katika asilimia 4.3 za mfumuko wa bei wa mwezi Agosti 2026, ikilinganishwa na mchango wa asilimia 1.5 katika mwezi Agosti 2025. Katika kipindi kama hicho mchango wa vyakula visivyochakatwa ulipungua kwa asimilia 0.8 kutoka asimilia 1.8, matokeo yake mfumuko wa bei ulihama kutoka kuchangiwa zaidi na chakula hadi kuchangiwa zaidi na shinikizo la bei la msingi (Kielelezo 2.1.6).

Kielelezo 2.1.6: Mchango Katika Mfumuko wa Bei

Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.


2.2 Sera ya Fedha

Benki Kuu iliendelea kutekeleza sera ya fedha ya kubana kufuatia uamuzi wa Kamati ya Sera ya Fedha wa mwezi Julai 2026 wa kuongeza kiwango cha Riba ya Benki Kuu hadi asilimia 6.25. Uamuzi huu ulilenga kudhibiti athari za awamu ya pili zinazoweza kutokea kutokana na ongezeko la bei za mafuta, mbolea na gharama za usafirishaji kufuatia mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati. Kwa muktadha huu, utekelezaji wa sera ya fedha ulilenga kuhakikisha riba ya mikopo ya siku saba baina ya mabenki inabaki ndani ya wigo wa asilimia 4.75 hadi asilimia 7.75.

Sera ya fedha kwa mwezi Agosti 2026 ilitekelezwa ili kuwezesha uwepo wa ukwasi wa kutosha katika sekta ya kibenki, ikiwezesha riba ya mikopo ya siku saba baina ya mabenki kubaki ndani ya wigo (Kielelezo 2.2.1). Benki Kuu imeendelea kusimamia ukwasi katika mfumo wa kibenki kwa kutumia mikopo ya muda mfupi na mauzo ya dhamana za serikali za muda mfupi. Kama ilivyokuwa katika mwezi uliotangulia, kulikuwa na ongezeko la mikopo ya muda mfupi kutoka Benki Kuu kufuatia baadhi ya benki kuwa na mahitaji makubwa ya ukwasi ili kukabiliana na upungufu wa muda mfupi (Kielelezo 2.2.2).


Kielelezo 2.2.1: Riba ya Benki Kuu na Wastani wa Siku 5 wa Riba ya Mikopo ya Siku 7

Asilimia



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 2.2.2: Mikopo ya Muda Mfupi Kwa Mabenki




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulipungua kidogo hadi asilimia 25.5 mwaka unaoishia Agosti 2026 kutoka asilimia 26.9 iliyorekodiwa mwezi uliopita, sanjari na mwelekeo wa sera ya fedha wa kubana (Jedwali 2.2.1 na Kielelezo 2.2.3). Ukuaji uliendelea kuchangiwa na mikopo kwa sekta binafsi, iliyokua kwa asilimia 33

kutoka asilimia 31.2 mwezi Julai 2026, ikiakisi ukuaji wa shughuli za uchumi (Kielelezo 2.2.4 na Kielelezo 2.2.5). Utekelezaji wa sera ya fedha unatarajiwa kupunguza taratibu kasi ya ukuaji wa mikopo.

Kielelezo 2.2.3: Mwenendo wa Ujazi Wa Fedha




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Jedwali 2.2.1: Ujazi wa Fedha na Vipengele Vyake

	Kiasi (Shilingi Bilioni)			Ukuaji kwa mwaka (%)		
Kipengele	Ago-25	Jul-26	Ago-26	Ago-25	Jul-26	Ago-26
Rasilimali halisi za nje	15,766.0	14,646.0	13,575.4	0.0	-6.9	-13.9
Rasilimali halisi za nje za Benki Kuu	13,933.2	14,562.1	13,730.9	10.7	4.9	-1.5
Rasilimali halisi za nje za mabenki	1,832.8	83.9	-155.5	---	-95.4	---
Rasilimali halisi za ndani	41,689.9	56,763.8	58,545.7	20.5	39.9	40.4
Madai rasmi ya ndani	54,561.2	65,914.8	68,067.2	15.7	25.4	24.8
Dhamana za Serikali zilizonunuliwa na benki za biashara	8,351.1	11,569.6	11,718.3	0.8	45.3	40.3
Mikopo kwa sekta binafsi	41,530.9	53,773.6	55,229.9	16.2	31.2	33.0
Rasilimali nyinginezo	-12,871.3	-9,151.0	-9,521.5	2.3	-23.6	-26.0
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	57,455.9	71,409.8	72,121.0	20.5	26.9	25.5
Amana za fedha za kigeni	13,696.3	16,771.0	16,043.5	14.1	22.8	17.1
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)	43,759.6	54,638.9	56,077.6	22.6	28.1	28.1
Amana zinginezo	16,357.2	19,984.5	20,484.7	20.2	21.8	25.2
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)	27,402.4	34,654.4	35,592.9	24.1	32.1	29.9
Ujazi wa fedha ulio kwenye mzunguko	8,036.4	8,933.6	9,120.0	10.1	10.0	13.5
Amana za hundi	19,366.0	25,720.8	26,472.9	31.0	42.0	36.7
Fedha za msingi (M0)	13,537.9	16,188.3	17,245.9	22.5	20.6	27.4


Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 2.2.4: Mabadiliko Katika Vyanzo vya Ujazi wa Fedha kwa Mwaka



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 2.2.5: Mwenendo Wa Mikopo Kwa Sekta Binafsi



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

Mikopo kwa sekta binafsi iliendelea kukua katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ambapo, shughuli uchukuzi na mawasiliano zilikuwa na ukuaji wa juu zaidi, zikifuatiwa na uchimbaji madini na biashara (Jedwali 2.2.2). Mikopo kwa ajili ya shughuli binafsi ambayo kwa kiasi kikubwa hugharamia shughuli za jasiriamali ndogo sana, ndogo na za kati iliendelea kuwa sehemu kubwa zaidi ya mikopo yote ikiwa ni asilimia 34.1, ikifuatiwa na shughuli za biashara na kilimo (Kielelezo 2.2.6).

Jedwali 2.2.2: Ukuaji wa Mikopo kwa Shughuli za Kiuchumi


Asilimia

Shughuli	Ago-25	Sep-25	Des-25	Mac-26	Jun-26	Jul-26	Ago-26
Uchukuzi na mawasiliano	18.8	17.4	29.4	39.5	59.5	66.0	77.2
Uchimbaji Madini	3.2	32.4	91.1	78.4	39.9	65.2	75.9
Biashara	29.2	24.8	49.7	43.3	46.4	43.5	47.1
Ujenzi	14.8	15.7	25.6	21.8	34.4	38.9	41.8
Kilimo	30.1	27.6	28.9	28.5	30.1	37.3	38.4
Shughuli binafsi	15.0	14.7	17.7	20.7	21.8	24.7	24.9
Hoteli na migahawa	11.4	16.3	2.5	4.4	0.9	25.1	24.6
Viwanda	3.4	0.1	-8.2	-4.9	8.3	5.1	12.9

Chanzo: Mabenki na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 2.2.6: Mgawanyo wa Mikopo Katika Shughuli za Kiuchumi

Asilimia



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

2.3 Viwango vya Riba

Viwango vya riba za mikopo na amana kwa kiasi kikubwa viliendelea kuwa tulivu mwezi Agosti 2026. Wastani wa riba za mikopo ulipungua kidogo hadi asilimia 15.05 kutoka asilimia 15.10 mwezi Julai 2026, wakati riba za mikopo kwa wateja wakubwa zilipungua hadi wastani wa asilimia 11.93 kutoka asilimia 12.04. Riba za amana za muda maalumu hazikuwa na mabadiliko zikiwa ni asilimia 8.78, huku riba za amana kwa wateja wakubwa zikiongezeka kidogo hadi asilimia 11.06, kutoka asilimia 10.99. Tofauti kati ya riba za mikopo na amana za mwaka mmoja ilipungua hadi asilimia 5.95 kutoka asilimia 6.2 mwezi uliotangulia (Jedwali 2.3.1).

Jedwali 2.3.1: Riba za Amana na Mikopo inayotolewa na Benki za Biashara

Asilimia

	Jan-26	Feb-26	Mac-26	Apr-26	Mei-26	Jun-26	Jul-26	Ago-26
Riba za amana	2.94	2.98	2.89	2.91	2.85	2.90	2.90	2.77
Riba ya mikopo - jumla	15.10	15.11	15.11	15.33	15.32	15.22	15.10	15.05
Riba za mikopo (mwaka 1)	15.49	15.41	15.45	15.31	15.38	15.38	15.54	15.31
Riba za mikopo (wateja wakubwa)	12.25	12.19	12.21	12.56	11.90	11.93	12.04	11.93
Riba za amana -jumla	8.33	8.32	8.33	8.54	8.43	8.69	8.78	8.78
Riba za amana (miezi 12)	9.70	9.82	9.60	9.81	10.17	9.72	9.34	9.36
Riba za amana (wateja wakubwa)	11.74	11.48	11.57	11.37	11.25	11.17	10.99	11.06
Tofauti kati ya riba za mikopo na amana	5.79	5.59	5.85	5.50	5.22	5.66	6.20	5.95

Chanzo: Mabenki na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania


2.4 Masoko ya Fedha

Soko la dhamana za Serikali

Minada ya dhamana za serikali iliendelea kuwa na mahitaji makubwa, huku dhamana za muda mrefu zikiendelea kuvutia zaidi wawekezaji, hali inayoakisi imani kubwa ya wawekezaji kuhusu matarajio ya hali ya uchumi.

Katika kipindi mapitio, Benki iliendesha minada miwili ya dhamana za muda mfupi zenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 580 kwa ajili ya kugharamia matumizi ya Serikali na kusimamia ukwasi katika uchumi. Minada ilipokea zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 981.7, sawa na uwiano wa zabuni dhidi ya kiasi kilichotolewa wa 1.7, huku zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 520.8 zikipokelewa. Wakati huo huo, wastani wa riba za dhamana za Serikali uliongezeka hadi asilimia 4.86, kutoka asilimia 4.74 mwezi Julai 2026 (Kielelezo 2.4.1).

Kielelezo 2.4.1: Mwenendo wa Minada ya Dhamana za Serikali




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Benki pia ilifanya minada ya hati fungani za miaka 15 na 25, yenye thamani ya shilingi bilioni 621.5. Minada hiyo ilikuwa na mahitaji makubwa, ikipokea zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 2,136.3– sawa na uwiano wa zabuni kwa mauzo wa 3.4. Kati ya zabuni zilizopokelewa, zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 595.4 zilikubaliwa. Wastani wa riba kwa hati fungani ya miaka 25 ulipungua hadi asilimia 11.48 kutoka asilimia 11.89 mwezi uliotangulia, huku wastani wa riba kwa hati fungani ya miaka 15 ukiongezeka kidogo hadi asilimia 10.55 kutoka asilimia 10.39, iliyorekodiwa katika mnada uliopita.

Soko la fedha baina ya mabenki


Soko la fedha baina ya mabenki liliendelea kuchagiza usambazaji wa ukwasi wa shilingi baina ya mabenki, na hivyo kuimarisha utekelezaji wa sera ya fedha. Jumla ya mauzo katika soko yalipungua hadi shilingi bilioni 4,566.2, kutoka shilingi bilioni 5,627 mwezi Julai 2026. Mikopo ya siku saba iliendelea kuchukua sehemu kubwa kwa takriban asilimia 47.8 ya jumla ya mauzo yote. Wastani wa riba katika soko ulifikia asilimia 6.67 ikilinganishwa na asilimia 6.57 mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.4.2).

Kielelezo 2.4.2: Mwenendo wa Soko la Fedha Baina ya Mabenki



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 2.4.3: Mwenendo wa Soko la Fedha za Kigeni



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Soko la fedha za kigeni

Soko la fedha za kigeni baina ya mabenki liliendelea kuwa na ukwasi wa kutosha ukichagizwa na mapato yatokanayo na mauzo ya dhahabu na mazao ya asili pamoja na kuimarika kwa shughuli za utalii. Katika mwezi Agosti 2026, jumla ya mauzo ya soko yalifikia dola za Marekani milioni 190.3, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 227.1 mwezi uliotangulia. Katika kukabiliana na mabadiliko makubwa ya thamani ya shilingi katika soko la fedha za kigeni, sambamba na sera ya ushiriki katika soko la mauzo ya fedha za kigeni, Benki Kuu iliuza jumla ya dola za Marekani milioni 45.4 (Kielelezo 2.4.3).

Wakati huohuo, shilingi ilishuka thamani kidogo dhidi ya dola ya Marekani, ikibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,657.01 kwa dola moja ya Marekani, ikilinganishwa na shilingi 2,653.52 kwa dola moja ya Marekani mwezi uliotangulia. Kwa ulinganifu wa mwaka kwa mwaka, shilingi ilishuka thamani kwa asilimia 6.7, ikilinganishwa na kuimarika kwa asilimia 0.5 mwezi uliotangulia. Mabadiliko hayo kwa kiasi kikubwa yalitokana na athari za rejea ambapo shilingi iliimarika kwa kasi mwezi Agosti 2025 hadi wastani wa shilingi 2,490.16 kwa dola moja ya Marekani, kutoka shilingi 2,666.79 kwa dola moja ya Marekani mwezi Julai 2025.


2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Mwezi Julai 2026, makusanyo ya mapato ya ndani yalikuwa asilimia 9.5, juu ya lengo la mwezi, yakifikia shilingi bilioni 3,502.2. Kati ya kiasi hicho, Serikali kuu ilikusanya shilingi bilioni 3,354.9 ikiwa ni sawa na asilimia 95.8 ya mapato yote.

Makusanyo ya kodi yaliendelea kufanya vizuri, yakifikia shilingi bilioni 2,877.0 sawa na asilimia 9.8 juu ya lengo la mwezi. Ufanisi huu ni matokeo chanya ya maboresho yanayoendelea katika usimamizi wa kodi na utii katika ulipaji wa kodi. Kwa upande mwingine, mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 477.9, pungufu ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 480.2 (Kielelezo 2.5.1).

Kielelezo 2.5.1: Mapato ya Serikali Kuu Mwezi Julai

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2026 ni za awali

Mwezi Julai 2026, Serikali imeendelea kuwianisha matumizi yake kuendana na mapato, ambapo ilitumia shilingi bilioni 3,572.4. Kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 2,779.5 zilitumika kwa matumizi ya kawaida, huku shilingi bilioni 792.9 zikielekezwa kwenye miradi ya maendeleo (Kielelezo 2.5.2).

Kielelezo 2.5.2: Matumizi ya Serikali Kuu Mwezi Julai

Shilingi bilioni



Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2026 ni za awali

2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa

Deni la Taifa (linalojumuisha deni la Serikali la ndani na la nje, na deni la nje la sekta binafsi) liliongezeka kwa asilimia 1.7 hadi kufikia dola za Marekani milioni 52,224.4 mwishoni mwa mwezi Agosti 2026. Kati ya kiasi hicho, asilimia 70.3 ilikuwa ni deni la nje (Kiambatisho, Jedwali A10).

Deni la Nje

Deni la nje, linalojumuisha deni la Serikali na sekta binafsi, lilifikia dola za Marekani milioni 36,731.5 mwishoni mwa mwezi Agosti 2026, juu zaidi kwa asilimia 0.8 toka mwishoni mwa mwezi Julai 2026. Deni la Serikali ni asilimia 83.7 ya deni lote la nje la Serikali, huku sehemu iliyobaki ikiwa ni deni la nje (Jedwali 2.6.1).

Mikopo ya nje iliyopokelewa mwezi Agosti 2026 ilikuwa dola za Marekani milioni 160.1, huku sehemu kubwa ikipokelewa na Serikali Kuu. Aidha, kiasi cha dola za Marekani milioni 139.1 kilitumika kulipia deni la nje, ambapo dola za Marekani milioni 69.2 zilitumika kufanya malipo ya mkopo mkuu.

Mashirika ya kifedha ya kimataifa yaliendelea kuwa wakopeshaji wakuu, yakichangia asilimia 59.5, yakifuatiwa na wakopeshaji wa kibiashara (Jedwali 2.6.2). Muundo ya deni kwa aina ya matumizi haukuwa na mabadiliko ambapo mikopo kwa ajili ya urari wa malipo ya nje na bajeti iliongoza, ikifuatiwa na mikopo kwa shughuli za usafirishaji na mawasiliano. Dola ya Marekani iliendelea kuwa sarafu kuu kwa asilimia 64.9 ya deni la nje, ikifuatiwa na sarafu ya Umoja wa Ulaya (Jedwali 2.6.3 na 2.6.4).

Jedwali 2.6.1: Mchanganuo wa Deni la Nje Kwa Kundi la Wakopaji

Dola za Marekani Milioni

	Ago-25		Jul-26r		Ago-26p	
Mkopaji	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)
Serikali Kuu	28,745.9	84.7	30,512.1	83.7	30,751.9	83.7
Deni ambalo halijalipwa	28,667.2	84.5	30,431.6	83.5	30,671.3	83.5
Malimbikizo ya riba	78.7	0.2	80.5	0.2	80.6	0.2
Sekta binafsi	5,192.9	15.3	5,942.2	16.3	5,979.6	16.3
Deni ambalo halijalipwa	5,088.1	15.0	5,732.0	15.7	5,751.2	15.7
Malimbikizo ya riba	104.8	0.3	210.2	0.6	228.4	0.6
Mashirika ya umma	1.3	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Deni ambalo halijalipwa	1.3	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Malimbikizo ya riba	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Jumla ya deni la nje	33,940.1	100.0	36,454.3	100.0	36,731.5	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali; na TANESCO, ATCL, TRC, TPA, TFC na DAWASA hazina deni la nje ambalo halijalipwa

Jedwali 2.6.2: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Kundi la Wakopeshaji

Dola za Marekani Milioni

	Ago-25		Jul-26r		Ago-26p	
Mkopeshaji	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)
Mashirika ya fedha ya kimataifa	20,014.9	59.0	21,733.4	59.6	21,867.4	59.5
Deni ambalo halijalipwa	19,992.8	58.9	21,709.0	59.6	21,842.7	59.5
Malimbikizo ya riba	22.1	0.1	24.4	0.1	24.7	0.1
Nchi washirika wa maendeleo	1,557.5	4.6	1,557.6	4.3	1,568.2	4.3
Deni ambalo halijalipwa	1,478.8	4.4	1,477.1	4.1	1,487.6	4.1
Malimbikizo ya riba	78.7	0.2	80.5	0.2	80.6	0.2
Benki za kimataifa za biashara	11,694.9	34.5	12,519.3	34.3	12,633.7	34.4
Deni ambalo halijalipwa	11,634.6	34.3	12,370.8	33.9	12,470.0	33.9
Malimbikizo ya riba	60.3	0.2	148.5	0.4	163.8	0.4
Mikopo ya mauzo ya nje	672.8	2.0	644.0	1.8	662.1	1.8
Deni ambalo halijalipwa	650.4	1.9	606.6	1.7	622.2	1.7
Malimbikizo ya riba	22.4	0.1	37.4	0.1	40.0	0.1
Jumla ya deni la nje	33,940.1	100.0	36,454.3	100.0	36,731.5	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r, inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na p, takwimu za awali

Jedwali 2.6.3: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Aina ya Matumizi

Asilimia

Shughuli ya uchumi	Ago-25	Jul-26^{r}	Ago-26^{p}
Urari wa malipo yote ya nje, na bajeti (BOP and budget support)	23.2	23.6	23.6
Usafirishaji na mawasiliano	21.0	21.6	21.8
Kilimo	5.1	5.2	5.2
Nishati na madini	11.9	12.7	12.6
Viwanda	2.9	2.6	2.7
Huduma za jamii na elimu	19.9	19.3	19.3
Fedha na bima	3.6	4.2	4.2
Utalii	1.8	1.6	1.6
Mali isiyohamishika na ujenzi	5.5	4.8	4.7
Mengineyo	5.1	4.3	4.3
Jumla	100.0	100.0	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r, inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na p, takwimu za awali

Jedwali 2.6.4: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Aina ya Sarafu

Asilimia

Sarafu	Ago-25	Jul-26^{r}	Ago-26^{p}
Dola ya Marekani	65.4	65.1	64.9
Sarafu ya umoja wa Ulaya (Euro)	17.9	18.2	18.4
Yuan ya China	6.6	6.7	6.7
Sarafu nyinginezo	10.1	10.0	10.0
Jumla	100.0	100.0	100.0


Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r, inamaanisha takwimu zilizobadilishwa; na p, takwimu za awali

Deni la Ndani

Deni la ndani la Serikali liliongezeka kwa asilimia 3.6 kwa mwezi, na kufikia shilingi bilioni 40,899.5 mwishoni mwa mwezi Agosti 2026, ikichangiwa zaidi na uuzaji wa hati fungani (Kielelezo 2.6.1 na Jedwali 2.6.5). Benki za biashara na mifuko ya hifadhi za jamii ziliendelea kuwa wakopeshaji wakubwa wa Serikali.

Kielelezo 2.6.1: Deni la Ndani la Serikali Kuu

Shilingi Bilioni



Chanzo: Wizara ya Fedha

Jedwali 2.6.5: Deni la Ndani la Serikali kuu kwa Vyanzo vya Mikopo

Shilingi Bilioni

	Ago-25		Jul-26		Ago-26^{P}	
Nyenzo	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)
Dhamana za serikali	32,048.0	85.8	35,530.5	90.0	36,722.5	89.8
Dhamana za serikali za muda mfupi	2,075.7	5.6	1,778.7	4.5	1,793.4	4.4
Hisa za serikali	135.7	0.4	135.7	0.3	135.7	0.3
Dhamana za serikali za muda mrefu	29,836.5	79.9	33,615.9	85.2	34,793.4	85.1
Vyeti vya ushuru	0.1	0.0	0.1	0.0	0.1	0.0
Deni lisilo na dhamana	5,261.8	14.2	3,941.7	10.0	4,176.9	10.2
Madeni mengine*	18.4	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Bakaa hasi	5,243.4	14.1	3,941.6	10.0	4,176.9	10.2
Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi)	37,309.8	100.0	39,472.2	100.0	40,899.5	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p, inamaanisha takwimu za awali; na madeni mengine yanajumuisha mkopo wa biashara na marejesho ya kodi ya ushuru

Jedwali 2.6.6: Deni la Ndani la Serikali Kuu kwa Kundi la Wakopeshaji

Shilingi Bilioni

	Ago-25		Jul-26		Ago-26^{P}	
Mkopeshaji	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)
Benki za biashara	10,558.3	28.3	11,450.6	29.0	11,599.3	28.4
Benki Kuu ya Tanzania	7,052.2	18.9	6,819.7	17.3	7,054.9	17.2
Mifuko ya hifadhi ya jamii	10,116.5	27.1	10,491.4	26.6	11,292.5	27.6
Kampuni za bima	2,001.9	5.4	2,063.0	5.2	2,050.4	5.0
Mifuko maalumu ya Benki Kuu	799.3	2.1	854.6	2.2	867.6	2.1
Wengine	6,781.7	18.2	7,792.9	19.7	8,034.7	19.6
Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi)	37,309.8	100.0	39,472.2	100.0	40,899.5	100.0


Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p, inamaanisha takwimu za awali; na "wengine" inajumuisha taasisi za umma, kampuni, watu binafsi, na wawekezaji wasio wakazi

Mwezi Agosti 2026, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 632.5 kutoka katika soko la ndani kupitia utoaji wa dhamana za Serikali kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 178.1 zilipatikana kupitia uuzaji wa dhamana za Serikali za muda mfupi, na shilingi bilioni 454.4 kupitia uuzaji wa dhamana za Serikali za hati fungani (Kielelezo 2.6.2). Wakati

huo huo, malipo ya deni la ndani yalifikia jumla ya shilingi bilioni 633.4, yakijumuisha shilingi bilioni 163.5 za marejesho ya deni la msingi na shilingi bilioni 469.9 za malipo ya riba.

Kielelezo 2.6.2: Dhamana za Serikali Zilizotolewa kwa Madhumuni ya Ufadhili wa Bajeti

Shilingi Bilioni



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Mwenendo wa sekta ya nje umeendela kuwa himilivu, ingawa mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati na matokeo ya mvurugiko wa masoko ya bidhaa duniani na usafirishaji vimeendelea kuathiri utendaji wake. Bei kubwa za bidhaa za petroli pamoja na bidhaa za kati ziliongeza ukuaji wa gharama za manunuzi zaidi ya ukuaji wa mauzo ya nje na hivyo kuongeza nakisi ya urari wa malipo. Matokeo yake, nakisi ya urari wa malipo ya nje iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 2,481.8 mwaka unaoishia Agosti 2026, kutoka dola za Marekani milioni 1,700.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2025 (Jedwali 2.7.1).

Akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa katika kiwango cha kuridhisha, kutokana na mapato ya mauzo ya nje na mpango wa Benki Kuu wa ununuzi wa dhahabu. Akiba ya fedha za fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,888.2 mwishoni mwa Agosti 2026, sawa na gharama za uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 4.2, ukiondoa uagizaji unaotokana na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje. Kiasi hiki ni juu ya lengo la kitaifa (Kielelezo 2.7.1).


Jedwali 2.7.1: Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali

Dola za Marekani Milioni

	Ago-25	Jul-26	Ago-26	Mwaka ulioishia Agosti			Mabadiliko ya asilimia
				2024	2025	2026^{p}	
Urari wa bidhaa	-327.7	-638.9	-478.0	-6,086.3	-4,340.3	-5,810.2	33.9
Zilozouzwa nje*	1032.4	1,116.8	1,080.1	8,055.2	9,981.2	11,960.8	19.8
Zilizonunuliwa nje	1,360.1	1,755.8	1,558.1	14,141.5	14,321.5	17,770.9	24.1
Urari wa huduma	454.51	563.0	627.1	4,127.4	4,193.6	4,757.2	13.4
Mapato	772.9	883.6	926.0	6,665.1	7,389.8	8,255.4	11.7
Malipo	318.4	320.6	298.9	2,537.7	3,196.2	3,498.2	9.4
Urari wa bidhaa na huduma	126.8	-75.9	149.2	-1,958.9	-146.6	-1,053.0	618.2
Bidhaa na huduma zilizouzwa nje	1,805.2	2,000.5	2,006.1	14,720.3	17,371.1	20,216.2	16.4
Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje	1,678.4	2,076.4	1,856.9	16,679.2	17,517.7	21,269.2	21.4
Urari wa malipo wa vitega uchumi	-176.3	-87.2	-111.3	-1,719.7	-2,026.5	-1,870.2	-7.7
Yaliyoingia	22.3	54.6	35.6	322.1	307.7	389.0	26.4
Yaliyotoka	198.6	141.8	146.9	2,041.8	2,334.2	2,259.2	-3.2
Urari wa uhamisho mali ya kawaida	24.8	54.8	58.2	597.0	472.2	441.4	-6.5
Iliyoingia	75.0	104.3	109.0	1,289.9	1,033.4	1,098.0	6.3
ambapo Serikali	3.2	0.0	1.6	125.0	100.6	38.1	-62.2
Iliyotoka	50.2	49.5	50.8	692.8	561.2	656.7	17.0
Urari wa bidhaa, huduma na uhamisho mali	-24.7	-108.3	96.0	-3,081.6	-1,700.9	-2,481.8	45.9

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p, inamaanisha takwimu za awali na *zinajumuisha marekebisho ya mauzo nje ya nchi ambayo hayajarekodiwa kikamilifu

Kielelezo 2.7.1 Akiba ya Fedha za Kigeni



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Mauzo ya nje


Mauzo ya nje ya bidhaa na huduma yaliongezeka kwa asilimia 16.4 hadi dola za Marekani milioni 20,216.2 kwa mwaka ulioishia Agosti 2026. Mauzo ya bidhaa nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 19.8 hadi dola za Marekani milioni 11,960.8, kutoka dola za Marekani milioni 9,981.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2025, ongezeko hilo lilitokana na mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani na bidhaa asilia (Kielelezo 2.7.2). Mauzo ya dhahabu yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 5,625, kutoka dola za Marekani milioni 4,321.5, yakichangiwa na bei nzuri katika soko la dunia na kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani. Mauzo ya dhahabu yalichangia karibu mbili ya tatu ya ongezeko la jumla la mauzo ya bidhaa nje ya nchi. Vilevile, mauzo ya bidhaa za viwandani yaliongezeka hadi dola za Marekani

milioni 2,213.4, kutoka dola za Marekani milioni 1,533.9, kutokana na ongezeko kubwa la mauzo ya chuma na bidhaa za chuma na vioo.

Ongezeko la mauzo ya bidhaa asilia yalichangiwa zaidi na tumbaku, chai na pamba. Kwa ulinganifu wa mwezi wa mwezi, mauzo ya bidhaa yalifikia dola za Marekani milioni 1,080.1 mwezi Agosti 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,032.4 mwezi Agosti 2025.

Kielelezo 2.7.2: Mauzo ya Nje ya Bidhaa na Huduma

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p, inamaanisha takwimu za awali

Mapato yatokanayo na huduma yaliongezeka kwa asilimia 11.7 hadi dola za Marekani milioni 8,255.4 kutoka dola za Marekani milioni 7,389.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mapato ya utalii na usafirishaji. Mapato ya huduma za usafirishaji yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 3,303.3, kutoka dola za Marekani milioni 2,612.5, yakichangiwa na kuongezeka kwa mapato ya usafirishaji wa mizigo kwenda nchi jirani (Kielelezo 2.7.3). Mapato ya utalii yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 4,389.7, kutoka dola za Marekani milioni 4,314.7, yakionesha uhimilivu wa shughuli za utalii. Kwa ulinganifu wa mwezi wa mwezi, mapato ya huduma yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 926 mwezi Agosti 2026, kutoka dola za Marekani milioni 772.9 mwezi Agosti 2025, yakichangiwa zaidi na mapato ya utalii.

Kielelezo 2.7.3: Mapato ya Huduma kwa Sekta

Dola za Marekani Milioni



Chanzo: Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Huduma nyinginezo zinajumuisha ujenzi, bima, huduma za fedha, mawasiliano ya simu, komputa na taarifa, ada za matumizi ya mali miliki ya kiakili, huduma za serikali, huduma binafsi, na huduma nyingine za kibiashara

Uagizaji wa Bidhaa na Huduma


Uagizaji wa bidhaa na huduma ulifikia dola za Marekani milioni 21,269.2 mwaka unaoishia Agosti 2026, ukiongezeka kwa asilimia 21.4 kutoka kipindi kama hicho 2025. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na uagizaji wa bidhaa za kati na bidhaa mtaji, huku bidhaa za petroli zikichangia sehemu kubwa ya ongezeko la uagizaji wa bidhaa za kati.

Uagizaji wa bidhaa za petroli uliongezeka kwa asilimia 51.7 hadi dola za Marekani milioni 3,425.6, kutoka dola za Marekani milioni 2,257.4, mwaka unaoishia mwezi Agosti 2025 (Kielelezo 2.7.4). Bidhaa za petroli zilichukua moja ya tatu ya ongezeko la gharama za bidhaa zilizoagizwa. Sambamba na ongezeko la kiwango cha bidhaa zilizoagizwa, malipo ya huduma za usafirishaji na gharama zinazohusiana na usafiri pia ziliongezeka, kwa kiasi kikubwa zikichangiwa na kupanda kwa gharama za mafuta duniani kufuatia mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati. Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, uagizaji wa bidhaa kutoka nje uliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 1,558.1 kutoka dola za Marekani milioni 1,360.1 mwezi Agosti 2025. Ongezeko hilo

lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa mtaji na bidhaa za mafuta ya petroli.

Kielelezo 2.7.4: Ulinganifu wa Uagizaji wa Bidhaa na Huduma

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p, inamaanisha takwimu za awali

Malipo ya huduma yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 3,498.2 mwezi Agosti 2026, kutoka dola za Marekani milioni 3,196.2 kipindi kama hicho mwaka 2025, yakichangiwa zaidi na malipo ya usafirishaji wa mizigo. Malipo ya usafirishaji mizigo yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 1,683.4, kutoka dola za Marekani milioni 1,300.4, yakionesha mahitaji makubwa ya uagizaji wa bidhaa na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji majini (Kielelezo 2.7.5). Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, malipo ya huduma yalifikia dola za Marekani milioni 298.9, kutoka dola za Marekani milioni 318.4 mwezi Agosti 2025.

Kielelezo 2.7.5: Malipo ya Huduma

Dola za Marekani Milioni



Chanzo: Uchambuzi wa Benki kuu ya Tanzania
Tanbihi: Huduma nyingine zinajumuisha ujenzi, bima, huduma za kifedha, mawasiliano ya simu, kompyuta na taarifa, ada za matumizi ya mali miliki ya kiakili,huduma za kiserikali,huduma binafsi, na huduma nyingine za kibiashara.

Nakisi ya urari wa mapato ya vitega uchumi ilipungua hadi dola za Marekani milioni 1,870.2 mwaka ulioishia Agosti 2026, kutoka dola za Marekani milioni 2,026.5 kipindi kama hicho mwaka 2025, ikichangiwa zaidi na kupungua kwa malipo yatokanayo na uwekezaji wa kigeni. Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi , nakisi ya urari wa mapato ya vitega uchumi ilipungua hadi dola za Marekani milioni 111.3 mwezi Agosti 2026, kutoka dola za Marekani milioni 176.3 mwezi Agosti 2025.

Ziada ya urari wa uhamisho wa mali wa kawaida ilipungua hadi dola za Marekani milioni 441.4 mwaka ulioishia Agosti 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 472.2 kipindi kama hicho mwaka 2025. Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, ziada iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 58.2 mwezi Agosti 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 24.8 mwezi Agosti 2025.

3.0 Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar

3.1 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei wa jumla ulipungua na kufikia asilimia 5.6 kwa mwezi Agosti 2026, kutoka asilimia 6 mwezi Julai 2026, ingawa ulikuwa juu ya asilimia 3.9 mwezi Agosti 2025 (Jedwali 3.1.1 na

Kielelezo 3.1.1). Ongezeko hilo lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa bei za vyakula, hususan mchele wa Mbeya, sukari, samaki na ndizi za kupika, pamoja na kuongezeka kwa gharama za usafiri kulikohusishwa na ongezeko la bei ya mafuta (Kielelezo 3.1.2).

Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, mfumuko wa bei wa bidhaa za walaji ulipungua kwa asilimia 0.2 mwezi Agosti 2026, ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 0.1 mwezi Agosti 2025, hali hii inaashiria kupungua kwa shinikizo la mfumuko ya bei wa muda mfupi huku mfumuko wa bei wa mwaka ukiendelea kubaki juu ya kiwango cha mwezi Agosti 2025.

Jedwali 3.1.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei


Asilimia (Kizio: Julai 2022 =100)

Kundi	Mizania	Mabadiliko kila Mwezi			Mabadiliko kila Mwaka		
		Ago-25	Jul-26	Ago-26	Ago-25	Jul-26	Ago-26
Vyakula na vinywaji visivyo na kileo	41.9	0.8	0.6	-0.4	4.8	10.9	9.6
Vinywaji vyenye vileo, tumbaku na madawa ya binadamu	0.2	-0.6	2.9	0.1	2.7	3.5	4.2
Mavazi na viatu	6.3	0.0	0.2	0.1	5.5	1.4	1.5
Makazi, maji, umeme, gesi na nishati nyingine	25.8	-0.9	-0.9	-0.5	3.0	0.5	1.0
Samani, vifaa vya nyumbani na matengenezo ya kawaida ya nyumba	4.8	-0.3	0.7	0.0	3.7	4.0	4.3
Afya	1.3	0.0	0.3	0.0	1.6	0.9	0.9
Uchukuzi	9.1	-0.2	-0.7	0.3	1.9	4.7	5.2
Taarifa na mawasiliano	4.2	0.0	0.9	0.0	2.7	0.3	0.3
Burudani, michezo na utamaduni	1.1	0.0	-0.2	0.4	4.3	2.7	3.0
Elimu	1.6	0.0	0.0	0.8	3.8	0.3	1.1
Huduma za migahawa na malazi	1.4	0.0	-0.2	0.0	1.6	6.2	6.2
Bima na huduma za fedha	0.5	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Huduma binafsi, ulinzi wa kijamii na bidhaa na huduma mbalimbali	1.7	0.4	0.9	0.0	5.4	1.6	1.1
Mfumuko wa bei wa jumla	100.0	0.1	0.1	-0.2	3.9	6.0	5.6
Mfumuko wa bei wa bidhaa za chakula	40.5	0.8	0.6	-0.4	4.2	11.1	9.8
Mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula	59.5	-0.4	-0.3	-0.1	3.7	1.9	2.2

Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar


Kielelezo 3.1.1: Mfumuko wa Bei wa Mwaka

Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

Kielelezo 3.1.2: Wastani wa Bei za Rejareja za Mafuta ya Petroli kwa Mwezi



Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar


3.2 Bajeti ya Serikali

Mapato ya Serikali pamoja na misaada yalifikia shilingi bilioni 251.3, mwezi Agosti 2026, juu ya lengo la mwezi kwa asilimia 10.4. Matokeo haya yalichangiwa na msaada wa kibajeti kutoka benki ya duniani. Mapato ya ndani yakifikia shilingi bilioni 198.1, ikiwa ni asilimia 78.8 ya mapato yote, sawa na asilimia 92.7 ya lengo la mwezi.

Mapato yatokanayo na makusanyo ya kodi yalikuwa ni asilimia 88.1 ya mapato ya ndani yakifikia shilingi bilioni 174.5, sawa na asilimia 88.1 ya lengo. Makundi yote ya vyanzo vya kodi hayakufikia lengo, isipokuwa kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa. Mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 23.6, juu ya lengo la mwezi kwa asilimia 38.2, kufuatia kuongezeka kwa makusanyo kutoka taasisi za Serikali (Kielelezo 3.2.1).

Kielelezo 3.2.1: Mapato ya Serikali

Shilingi Bilioni




Chanzo: Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar
Tanbihi: Kodi nyingine zinahusisha tozo za hoteli, tozo za wasindikiza wageni, stampu za tozo, tozo za huduma za viwanja vya ndege na bandari, tozo za maendeleo ya barabara na petroli

Matumizi ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 459 mwezi Agosti 2026. Kati ya kiasi hicho, asilimia 73.3 zilitumika kwenye miradi ya maendeleo, na kiasi kilichobakia kilielekezwa kwenye matumizi ya kawaida za Serikali (Kielelezo 3.2.2).

Kielelezo 3.2.2: Matumizi ya Serikali

Shilingi Bilioni



Chanzo:Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar
Tanbihi: Matumizi mengine yanahusisha uhamisho wa fedha, malipo ya riba ya deni la ndani, huduma za mfuko mkuu wa serikali na tozo zingine.

3.3 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Urari wa malipo uliongezeka kwa asilimia 19.3 na kufikia dola za Marekani milioni 953.7 katika mwaka ulioishia Agosti 2026, kutoka dola za Marekani milioni 799.3 kipindi kama hicho mwaka 2025 (Jedwali 3.3.1). Matokeo haya yalitokana na kuongezeka kwa mapato ya huduma, yaliyoendelea kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii na kupungua kwa malipo ya huduma.

Jedwali 3.3.1: Urari wa Malipo

Dola za Marekani Milioni

Maelezo	Ago-25	Jul-26	Ago-26	Mwaka unaoishia Agosti 2025	Mwaka unaoishia Agosti 2026[p]	Ongezeko/ Upungufu (Asilimia)
Urari wa bidhaa (Halisi)	-47.7	-55.9	-56.1	-514.2	-769.8	49.7
Zilizouzwa nje	1.8	3.3	1.9	32.5	69.2	---
zilizonunuliwa kutoka nje	49.5	59.2	58.0	546.8	839.0	53.4
Urari wa huduma (halisi)	182.8	191.0	221.4	1,420.3	1,707.2	20.2
Mapato	191.8	196.0	226.3	1,521.6	1,777.8	16.8
Malipo	9.1	5.0	5.0	101.3	70.5	-30.3
Urari wa bidhaa na huduma (halisi)	135.1	133.7	163.5	789.1	935.6	18.6
Bidhaa na huduma zilizouzwa nje	193.6	199.4	228.2	1,554.2	1,847.0	18.8
Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje	58.6	64.2	63.0	648.0	909.5	40.4
Urari wa mapato ya msingi (halisi)	0.2	2.2	2.6	9.1	14.6	59.9
Yaliyoingia	0.3	2.4	2.7	12.9	16.5	27.3
Yaliyotoka	0.1	0.1	0.1	3.8	1.8	-51.5
Urari wa uhamishaji Mali (halisi)	0.0	0.7	0.9	1.0	3.5	244.7
Iliyoingia	0.0	0.7	0.9	2.1	4.1	93.8
Iliyotoka	0.0	0.0	0.0	1.1	0.7	-40.5
Urari wa Bidhaa,huduma na uhamishaji mali	135.3	136.6	166.9	799.3	953.7	19.3

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania, benki na uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.
Tanbihi: p inaashiria Takwimu za awali; fob, 'Mzigo ndani ya chombo

Mauzo ya nje

Mauzo ya bidhaa na huduma yaliongezeka kwa asilimia 18.8 na kufikia dola za Marekani milioni 1,847 mwaka ulioishia Agosti 2026, ikichangiwa zaidi na mauzo ya huduma zinazohusiana na utalii (Jedwali 3.3.1). Mauzo ya bidhaa nje ya nchi yaliongezeka zaidi ya mara mbili, hadi dola za Marekani milioni 69.2, yakichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa asilia hususan karafuu (Jedwali 3.3.2).

Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, mauzo ya bidhaa na huduma yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 228.2 mwezi Agosti 2026, kutoka dola za Marekani milioni 193.6 mwezi Agosti 2025.

Jedwali 3.3.2: Uuzaji wa Bidhaa

Dola za Marekani Milioni

Maelezo	Uniti	Ago-25	Jul-26	Ago-26	Mwaka unaoishia Agosti 2025	Mwaka unaoishia Agosti 2026[p]	Ongezeko/ Upungufu (Asilimia)
Mauzo ya nje ya bidhaa za asili							
Karafuu							
Thamani	Dola ya Marekani	-	824.0	216.2	3,574.0	42,494.6	---
Kiasi	000' kwa Tani	-	0.8	0.1	0.8	7.2	---
Bei kwa uniti	Dola ya Marekani/Tani	-	1,089.1	3,891.4	4,669.5	5,936.7	27.1
Mauzo ya nje ya bidhaa zisizo za asili							
Mwani							
Thamani	Dola ya Marekani	160.7	152.7	135.0	3,079.7	1,311.4	-57.4
Kiasi	000' kwa Tani	0.4	0.3	0.2	5.6	2.2	-60.7
Bei kwa uniti	Dola ya Marekani/Tani	404.7	495.5	647.9	550.4	596.9	8.5
Bidhaa za viwandani	Dola ya Marekani	1,595.2	1,734.0	1,143.7	17,329.0	11,574.6	-33.2
Bidhaa za samaki	Dola ya Marekani	35.2	326.2	49.3	730.5	1,052.5	44.1
Mauzo ya nje ya nchi kwa bidhaa nyingine	Dola ya Marekani	0.2	306.9	330.6	7,834.1	12,756.9	62.8
Jumla Ndogo	Dola ya Marekani	1,791.3	2,519.7	1,658.6	28,973.3	26,695.4	-7.9
Jumla Kuu	Dola ya Marekani	1,791.3	3,343.7	1,874.8	32,547.3	69,190.0	---

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Uagizaji wa bidhaa na huduma

Uagizaji wa bidhaa na huduma uliongezeka kwa asilimia 40.4 na kufikia dola za Marekani milioni 909.5 mwaka ulioishia Agosti 2026, ukichangiwa zaidi na uagizaji wa bidhaa mtaji na malighafi(Jedwali 3.3.1). Uagizaji zaidi wa bidhaa za mitaji, ulichangiwa na uagizaji wa mashine na vifaa vya mitambo (Jedwali 3.3.3). Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, uagizaji wa bidhaa na huduma uliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 63 mwezi Agosti 2026, kutoka dola za Marekani milioni 58.6 ikilinganishwa na mwezi kama huo mwaka 2025.

Jedwali 3.3.3: Uagizaji wa Bidhaa

Dola za Marekani Milioni

Maelezo	Ago-25	Jul-26	Ago-26	Mwaka unaoishia Agosti 2025	Mwaka unaoishia Agosti 2026P	Ongezeko/ Upungufu (Asilimia)
Bidhaa za mtaji	8.7	16.5	16.7	71.8	224.2	---
Mitambo na vifaa vya kimitambo	5.2	7.2	7.0	28.3	81.5	---
Vifaa vya usafirishaji viwandani	0.8	5.1	5.0	23.0	76.2	---
Mashine na vifaa vya umeme	2.0	3.2	3.2	13.5	49.3	---
Bidhaa nyingine za mtaji	0.7	1.0	1.0	7.0	17.3	---
